**MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**102/1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. Insha ichukue muundo wa barua rasmi. (Barua kwa mhariri)
   Anwani ya pili iwe kwa mhariri ...
2. Mwanafunzi azingatie hoja zifuatazo.
   (i) Aonyeshe jinsi mazingira yanaharibiwa kama vile;
   - Ukataji wa miti.
   - Viwanda vinavyotoa gesi chafu hewani.
   - Mbinu za kilimo zinazochafua mito. Mfano dawa za kunyunyizia mimea.
   - Urudikaji wa taka katika sehemu ambazo hazistahili.
   - Uchomaji wa makaa.
   - Ufugaji mfano ufugaji wa mifugo katika maeneo ambayo hayastahili kama vile misitu.
   - Kuelekeza uchafu mitoni. Mfano viwanda, kufua nguo.

   *(Hoja zozote tatu)*

   (ii) Aonyeshe jinsi ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira.
   - Kukashifu ukataji wa miti.
   - Viwanda kuhakikisha kwamba gasi inasafishwa kabla ya kuachilia hewani / angani.
   - Kuelimisha wakulima kuhusu mbinu zinazofaa za ukulima.
   - Serikali kuwachukulia hatua kali wanaochafua mazingira,
   - Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuyatunza mazingira.

   *(Hoja zozote tano)*
   *Mwalimu akadirie hoja zingine.*

2. Madhara ya mitandao ya kjamii.
- Uzembe miongoni mwa wanafuzi.
- Udanganyifu katika mitihani.
- Kutumia muda / wakati vibaya (kupoteza wakti) wa masomo.
- Kupotosha maadili (ukosefu wa nidhamu shuleni)
- Kujihusisha na marafiki wabaya (wanaopotosha)
- Wizi wa pesa ili wanafunzi waweze kununua simu na malipo ya mtandao.
- Kushawishiwa kujiunga na vikundi haramu kama vile kigaidi hivyo basi kukatiza masomo.

   *(Hoja zozote tano)*
   *Mtahini akadirie hoja zingine.*

3.
- Mlezi akiogopa kumrudi mwanawe ndiye atakayejuta kwa kudorora kwa tabia kwa mwanawe.
- Kisa kihusu majuto aghalabu kwa mlezi aliyetelekeza ulezi wa mwanaye.
- Kisa kidhihirishe jinsi ambavyo mzazi alikosea kumwelekeza mwanawe alipokuwa akifanya maovu na jinsi mzazi alivyoathirika baadaye.

4.
- Mtahiniwa atunge kisa na kuazia na maneno aliyopewa. Asipofanya hivyo amejitungia swali hivyo
- atuzwe 02.
- Atumie usimulizi rejeshi kufafanua matukio kabla ya mlipuko.
- Aonyeshe mlipuko ulikuwa umesababishwa na nini na aeleze jinsi alijinusuru.

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479